




Umewahi Kuiskia...

# Habari Njema!



**Dhambi Zako Zimesamehewa!!**



## Msamaha Wa Dhambi

Mbele Yesu hajaenda mbinguni, aliwapa wafuasi wake amri hii:

“Enendaeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injiri kwa kila kiumbe.”—Marko 16:15

Luka naye aliandika hivi:

“Akawambia, Ndivyo ilinyoandikwa, kwamba kristo atateswa na atafufuka siku ya tatu, na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa Jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzianza tangu yerusalemi.”—Luka 24:46-47

Kufuatana na mashahiri hayo, malengo ama shabaa yakeni hii ndiyo amri Yesu aliyotoa kwa. Kanisa lake kuihubiri injiri Siku ya pentekositi Petro alisema:

“Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho mtakatifu.”—Matendo 2:38

Na wakati injiri itawaendea mataifa na kwanza Petro kairudia amri ya Kristo:

“Akatuagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe mhukumu wa walio hai na wafu; na manabii wote humushuhudia ya kwamba kila amwambiniye atapata ondoleo la dhambi zake.”—Matendo 10:42-43

Paulo akatoa ujumbe huu pia, baada ya kusoma maandiko yasemayo kwamba Yesu ndiye Kristo na mwokozi wetu,

“Basi na ijulikan ya kwa kila mtu nanyi ndugu zangu, ya kuwa kwa Huyo munayisikia injili na kuhubwa msamaha wa dhambi.”—Matendo 13:38

Kumbuka ya kuwa tumeokolewa Kwa neema Na tukishangaa Sana uhusiyano wetu na watu wengine wakua mzuri chini yahayo tunaanza kuwatendea wengine sawasawa na vile Mungu anavyotutendea. Paulo alisema “Sote tutapita mbele ya hukumu ya Mungu kwenye kiti chake Kristo” 1 Wakorinso 5:10”

Kama utikufu na imani vyenu havizidi vya mfarisayo na hamtaingia katika ufalme wa mbinguni. Matayo 5:20. Tunahitaji utukufu kwa matendo yetu wala si kwa maneno tu. Lakini swali ni hili. Kitu gani ambacho kitatuwezesha utukufu huo? Msamaha wa dhambi pekee ndio utatuwezesha kupitia habari njema.

Hatapotea mtu yeyote ambaye anategemea msamaha wa dhambi hivi hufanva jambo nzuri na atazaa matunda mema. Yumkini kazi yake isitambuliwe Kwa haraka, hata naye mwenyewe; lakini Mungu huona yoyote atendayo Kwa kuwa maisha yake ni ushuhuda wa msamaha wa dhambi kwa imani yake. Naamini msamaha wa dhambi.

Hasemi hivyo kwa kuwa tunaye roho mtakatifu. Ambaye anatumia na dhambi? Husema hivyo kwenye sura ya 8 lakini kwenye sura ya sita anasema “Dhambi haitatutawala kwa kuwa hatupo chini ya sheria, tupo chini ya neema”

Na kwa njia nyingine dhambi itatutawala wakati hatuna neema ya Mungu. Tupo chini ya sheria wakati tunawaza ya kuwa tupo na uhuru wa kujitukuza wenyewe.

Kanisa la mafarisayo walifikiri ya kwamba wanaweza kujitakasa. Na tukifwata nyayo zao twajidanganya, hatuishi chini ya nsamaha wadhambi, nayo dhambi itatutawala sisi. Tunapotambua nguvu na utukuvu wake kristo vimo ndani yetu, na nguvu zake shetani zimeshindwa kwakuwa uweza wa nguvu za Kristo wavunja nguvu za shetani? Kama Paulo aliwasema “Hawana hatia wenyekuwa chini ya neema yake Mungu” Kristo anasimama kwenye na fasi yao isiyu ya utukuvu. Mungu huwatizama wenye utukuvu bila dhambi kabisa na wanaweza kumtumikia Bwana.

Luther alisema hata matendo yetu mazuri yahitaji msamaha ili yakubaliwe mbele ya Mungu. Alamuomba Bwana kumsamehe dhambi juu ya ombi zake juu zenye hazikuwa sawasawa. Mwenye msamaha anawo ulimzi na neema ya Mungu. Huishi kama maskini chini ya jua. Akimlilia Mungu mchana na usiku “nisamehe mimi mwenye dhambi” na baadaye nitaishi kwa amani na watu wengine..

Mungu wakati wahukumu ataichunguza mioyo ya watu wala si matendo yao ya mwili. Mfano ni wanye kuamkia kanisani wanao toa sadaka na zaka kwa hekalu, watapoteza nafasi zao mbinguni. Matayo 23:23 Yumkini kuwa na mtumishi ndani ya kanisa walakini, mwenye tabia mbovu, mwenye hana msamaha, bila huruma na mwenye moyo wa jiwe. “Wasimtukane mtu yeyote, wasiwe wgomvi, wawe wema. Lakini wema wake mwokozi wetu kwa wanadamu ulipomfunuliwa alitukoa si kwa matendo yetu bali kwa neema yake” Tito 3:2-4



Wakati musherekeapo meza ya Bwana, msamaha wa dhambi husherekewa pia. Kristo akitwaa kikombe na akasema,

“Nyweni nyote, kwa maana lili ndilo agano la damu yangu imwangikayo kwa ondoleo la dhambi zenu.”—Matendo 26:27-28

Musamaha wa dhambi ni shina la injiri. Yesu kamwambia kiwete, ‘Mwanangu dhambi zako zimesamehewa.’ (Marko 2:5). Na kwa Mariamu alievunja chupa la manukato katika Nyumba ya Simoni kristo alimwambia:

“Dhambi zako ambazo ni nyinpi zimesamehewa kwa kuwa umependa sana; lakini anaye zambi ndogo naye husamehewa kidogo na kwahio hupenda kidogo; kisha alimwambia mwanamke: Dhambi zako umesamehewa, ndipo wale walioketi chakulani pamoja naye walianza kusema mioni mwao, Nina huyu hata asamehe dhambi? Akamwambia mwanamke imani yako imekuokoa enenda zako kwa amani.”—Luka 7:47, 50

Wokovu na musama wa zambi vyatumika pamoja, walakini si wokovu pekee yake kwa kusamehewa. Paulo kawambia Waefeso,

“Kwa damu yake Yesu, tumepata msamaha wa dhambi zetu kwa neema yake Bwana.”—Waefeso 1:17

Msamaha wa dhambi ni funzo kubwa kwa dini ya Kristo. Mtume aliegemeza mafundisho yake kwa kusema Kusamehewa Dhambi Ili Kupata Wokovu.

Namwamini Mwenyezi Mungu Baba,

muunbaji wa pekee Yesu Kristo, Bwana wetu, aliezaliwa kwa nguvu ya roho mtakatifu na Bikira Maria, kateswa na Ponsiyo Pilato, kasurubiwa na akafa na kazikwa kaburini.

Kafufuka toka kaburini kwa siku ya tatu. Nakaenda mbinguni na akaketi kwa mkono wa kuume wa Mungu, na atarejea tena kuwahukumu walio kufa na waliwo hai.

Naamini roho mtakatifu na kanisa tukufu la Kristo, meza ya Bwana; msamaha wa dhambi, ufufuo wa mwili na uzima wa milele.

“Naamini msamaha wadhambi “Dhambi husamehewa katika jina la Yesu. Na kwa ajili ya mateso alioyapata Mwenye imani ataokolewa na apate uzima wa milele.

Na kwa hivyo mwenye kusamehewa ameokolewa na anao uzima wa milele. Hakuna mtu ambaye baada ya kusoma neon la Yesu Kristo na manabi, mtume wake awezae kukana ukweli kana kamba ni nguzo ya injili inayo hubiriwa na iletayo uzima na nghuvu tangu myaka ya sitini kuanza na mitume wa YESU KRISTO.

## Nguvu Za Injiri

Zaburi ya 32 ni moja wapo wa Zaburi alizozitumia mtume Paulo kwa kitabo cha Warumi 4:6-8.

Heri aliyesamehewa dhambi, na kusitiriwa makosa yake.

Heri mtu ambaye Bwana asiyemhesabia zambi zake na upotovu wake, mtu.

Ambaye rohoni mwake hamna hila. Niliponyamanza mifupa yangu ilichakaa kwa kuuguwa kwangu mchana kutwa.

Kwa maana mchana na usiku, mkono wako ulinilimea. Jasho langu likakauka hata likawa Kama inchi kavu ya kasikazi.

Nali kujulisha dhambi yangu wala sikuficha upotovu wangu. Nilisema, nitayakiri maasi yangu kwa Bwana nawe ukanisamehe upotovu wangu na dhambi yangu.

Kwa hiyo kila mtu mtauwa akuombe wakati unapopatikana. Hakika maji makuu yafurikapo hayatamfikia yeye.

—Zaburi 32:1-6


Hivi ndivyo watu wa Mungu wataomba Wenye roho wake, Mtu heri (kwa kuwa ni yule ambaye Amebarikiwa. Ni mtu ambaye dhambi zake zimesamehewa. Na mwenye kupatikana bila hila (1-2) yaani ambaye atamlaki Bwana ajapo (Ufunuo 14:5) ni wale waishio bila kudanganya; wanaohitaji msaada wa mbingu na neema yake. Waishio kwa msamaha wa dhambi.

Yokaana alionya hivi:

“Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo ndani mwetu. Tukuziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki atundelee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote”—1 Yokaana 1:8-9



Tendo Lake Mwanamke, halikuwapendeza waliopo chakulami, hata walikasirika. Lakini Yesu ndiye akimu na kawapa mfano wahukumu la mwisho na akasemwa. “Mwacheni, mbona mnataabisha, aminitendea kitendo chema” Marko 14:6 Alisema jambo hili lilikuwa tendo jema, kwa nini? Kwa sababu tendo hilo lilionesha hitaji la msaada kutoka mbinguni. Alisamehewa mingi na kwa hivyo alipenda kwa upenda mkubwa (Luka 7:47).



Hakuna jambo lolote hata ndogo linalo watendewa watoto wa Mungu ambalo halitakumbukwa (Marka 9:41). Yumkini, kusahauliwa Kama watendaji walikuwa wakitaka sifa na kama Laodikia mwenye hakuwa na hitaji la msamaha wa dhambi zake!

Hakuna jambo ambalo lipenyalo Kama kusamehewa na upendo wa Kristo. Upendo huu hauwezi; Kushindwa msamaha wa mtu, yeyote kupitia mtu huyu msamaha wa dhambi umetangazwa. Matendo 13:38 Muandishi wa kitabo cha Waebrania alisema Nia ya pashwa kusafishwa kutoka kwenye Matendo maovu. Damu yake Kristo pekee iliyomwangika ambayo yaweza kusafisha dhambi na hio ambayo itatuwezesha kuishi mbele yake Mungu bila mawa. Na kwa hayo hatutaweza kumtumikia Mungu bila kupata msamaha wa dhambi. Msamaha huu ni jambo la mhimu sana linatuwezeshalo kutotenda dhambi tena. Zamiri ni kiwanda ambacho

cha tuonesha dhambi. Paulo ajisema “Hata kamwe dhambi haiwezi kutawala juu yetu” Warumi 6:14.


Wote wemepungukiwa na upendo wa Mungu kufuatana na dhambi zao. Na "Hukumu yawangoja isipokuwa Mungu kwingilia kati kwa neema yake. Sote tupo mbele ya kiti cha hukumu lake Mungu tukiomba kuhurumiwa. Kinyume cha, mfarisayo, mwenye deni asiehurumia mtumwa mwenziwe, pamoja na mtoto aliebacki nyumbani ambao hakuwa na huruma, wote walikuwa hawana huruma kwa wenziwo. Hivyo hivyo hawakupewa msamaha na huruma hiyo.

Kwa kweli moyo wa Binadamu hauna msamaha. Hauna huruma na sijambo kwa binadamu mwenye hana huruma kwa ndugu yake.

Kwanini walihekumiwa; Mfarisayo, Mwenye deni la mfalume na mkubwa wake mtoto mpotevu? Walikataa roho ya kuwasamehe wenziwo. Hawakutambua hitaji lao. Hukumu yanye bila huruma itahukumiwa vile vile bila huruma. Jakobo 2:13.

Laodikia ni mfarisayo aliyesahau kwamba Mungu wa Biblia ni mwenye haki na huruma. Mtenda maajabu, yasiosio tendwa na yeyote, mtu yeyote anayemkaribisha mwenye dhambi. (Warumi 4:5, Luka 15:2, Matayo 9:13) Wahitaji, maskini, walikotiliwa mbali, na wale ambao wanahitaji neema yake Mungu na tayari kukaribia mbinguni; na wale M

## Matunda Ya Injiri



Tunapashwa kusonga mbele tukitenda matendo mema. Lakini si matendo hayo ambayo atakuokoa kwenye hukumuyetu. Kwa kuwa wengi watahukumiwa Pasipo kutazama matendo yao mema na Bwana atawambia "Ondokeni mbele yangu kwa kuwa siwajuwe ninyi" Matayo 7:23 Kwa kuwa

jambo ambalo wanadamu hulisifia ni chukizo kwa Mungu. (Luka 16:15) Nakwa hivyo, Mungu anatoa hukumu yake vipi? Ninani na matendo gani ambayo atakaye yakubali Mungu?

Na tazama mwamke mmoja wa mji ule alikuwa mwenye dhambi aliopata habari ya kuwa ameketi chakulani kwenye nyumba ya mfarisayo alileta chupa la marimari yanye marhamu, akasimama nyuma karibu na miguu yake akatoa machozi na kumdongosha miguu yake Yesu, alipangusa kwa nywele zake na kwibusu na kwipakaa yale marhamu!—Luka 7:38-39

Hapa tunazo njia mbili, 1- Kwanza msamaha wa dhambi ni nguzo ya injili. 2- Pili kuziungama dhambi kwa kristo wakati tunapohitaji msamaha wa dhambi, na kwa hayo tunao uzima wa milele na tumeokolewa.

Muumba wetu hawezi kunyenyekea kwa ajili ya dhambi zetu. Leo Mungu anatuomba sawawa na Adamu babu wetu mbele ya dhambi jambo moja; utukufu na utiifu wa amri zake ili tuepukane na deni la dhambi, pia inatubidi tuyatimize matakwa ya. Yake Mungu. Kuna mtu ambaye ameambatana na roho wa Mungu anayeweza kushindwa na amri hizo, kamwe, Yakobo alisema "Sote tumepungukiwa na utukufu wa Mungu, na sote twatenda dhambi na tukisha tenda maovu hayo Yesu hutwambia yatupasayo; Kuziungama dhambi zetu kwa kua tumekua kana kwamba hatuna faida. Luka 17;10. kama mtu anasema hana dhambi mtu huyo ni muongo kweli hayimo ndani mwake. Daudi alitukumbuka kwenye ombi lake 'Wala usimihukumu mtumishi wako kwa maana hakuna aliye hai alie haki Zaburi 143 ;2.

Baada ya kwosha miguu yao mtume, kwa chakula cha mwisho, lango lake mwokozi lilikuwa kuhitaji kuosha na msamaha. "yokaana 13:3-15) Kristo hakutufunza kuomba mara moja, si sasa na baadaye lakini, wakati tuombapo chakula cha kila siku' Utusamehe makosa yetu kama tuyovwasamehe wale wanao tukosea pia." Matayo 6:12

Amri yote inatimizwa kwa jambo moja "Umpende jirani yako kama mwenyewe." Wagalatiya 5:14 Yesu alisema:

"Utampenda Mungu Bwana wako kwa moyo wako wote, na akili yako, na nguvu zako zote. Hii ndio amri kubwa naya kwanza; naya pili kama hiyo, Utampenda jirani yako kama mwenyewe; hizi zinginezo hutimiya ndani ya hizi mbili"—Matayo 22:37, 40

Sheria huhitaji upendo nakumfanya Mungu kuwa wa kwanza kwa kila kitu kipendezacho. Inatupasa kujitia kwa kila wakati. Heshima na shukrani ni vyake milele. Na jirani yako kumtiya mbele kwa kila jambo. Tunapashwa kumpenda Kama tujipendavyo wenyewe. Paulo alisema: "Msiwe na deni la mtu lolote isipokuwa kupendana, kwa maana ampandaye mwenzake ameitimiza sheria yote" Warumi 13:8

Watu wengi huogopa kutegemea msamaha wa dhambi wakiofia matendo yao na mawazo ya kua hawataingia mbinguni kulingana na dhambi. Tunahitaji dini yenye kweli ambayo itatuondoa chini ya utawala na utawala wa dhambi. Na kipawo cha roho kina kuja na msamaha wa dhambi.

Petero alipokwa akihubili msamaha wa dhambi kwa Cornelio, roho aliwashukia walio sikia neon lake: (Matendo 10:44; 2:38)

Popote roho wa Mungu ajapo, huleta na matunda yake. Na kwa kushinda dhambi lazima msamaha wa dhambi upate msitale wa kwanza katika maisha ya wafuasi wake kristo. Wakati watoto wa Mungu bado kuinua msamaa ha wa dhambi hawatapota ushindi.

## Roho Wawo Mafarisayo

Kanisa tajiri, mimejitajirisha, wala sina haja ya kitu, nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge “ (Ufunuo 3:17) kanisa hili la Ladikia ni sawa sawa nala Mafarisayo. Wakati mwingine tunawachekelea kwa Matendo yao bila kujitambua sisi wenyewe.

Mfano ya Yesu iliwatambua Mafarisayo na maovu yao, si kwa sababu hakuwapenda walakini kuwafunza na kujua uovu wao na watubu!! Na mfano hii ilileta ujumbe mkubwa kwa kanisa la Laodikiya:

**Mfano Wa Mfarisayo Na Mtoza Ushuru.** “Watu wawili walienda kuabudu kanisani, Mfarisayo na Mtoza ushuru. Bila kusita Mfarisayo alikuwa wa Laodikiya; alipoomba Alimushukuru Mungu nakatowa mali yake kama shukrani kwa matendo yake Mungu mema. Juu ya maisha yake.” Luka 18:11 Mfarisayo huyu alikosa kitu kimoja, na nikitu gani? “Hakuomba msamaha wa dhambi

zake, alikuwa hana haja nao. Na kwa sababu hakuhitaji msamaha Hivyo hivyo hakuutoka na kumsamehe maskini mtoza ushuru na kamuangalia kwa jicho baya. Hakuomba na hakutaka kuwasamehe wenzake. Kwa nje alionekana mtakatifu kabisa na alikua hahitaji chochote. Dini huenda mbali na utakatifu wa nje Maandiko husema; “Wahitaji kweli ndani ya moyo” Zaburi 51:6. Mfarisayo huyu hakuomba neema ya Bwana na hakwa na neema na hakuomba wenzake na kwa hivyo alisimama mbele ya hukumu ya Mungu bila huruma. (Luka 18:14)

## Mfano Wa Mwenye Deni.

Tukiangalia tena Laodikia katika mfano huu kweli. Mtu aliekuwa na deni la Mfalume; Aliposhindwa kulipa,; Mfalume akaamuru auzwe na mali yake yote lakini akamusii na kumuomba, Bwana naomba unionee huruma Ni mda kitambo nami nitakulipa yaliyo yako: mfalume kamuonea huruma na kamusame. Matayo 18:26.

Baadaye mtumwa alipoondoka kwenye jumba la Mfalume. Kamkuta mtumwa mwenziwe ambaye anamdayi. , kamshika shingoni na kumdayi akisema”Lipa pesa zangu” Matayo 18:26.

Mtumwa huyu kamsihii Sana. Akitumia yale maneno aliyoyatumia mwenyewe mbele ya mfalume, lakini hakumsikiza. Walio yatazama hayo yote walimpasha Mfalume. Mfalume alikasirika sana na kamwambia “Mtumishi mbaya wewe “mimi nimekusamehe deni lote, kwa sababu gani hukusamehe mtumwa mwenziwo na kumuhurumia yeye? Matayo 18:32,33



Tatizo lake la kwanza lilikua nini? Kuwa na huruma naye baadaye angelipa. Aliomba msamaha wa mda fulani na kulipa kufuatana na njia zake mwenyewe. Alitaka kusamehewa bila yeye mwenyewe kumsamehe mtumwa mwenzake baadaye naye angemsamehe mwenzake.

## Mfano Wa Vijana Wawili Mtoto Mupotevu

Katika mfano huu, mdogo alienda nchi za mbali na akai kwenye nyumba ya nguruwe akifanya lalote aliloambiwa. Ili kupata chakula cha kila siku. Muishowa Baba watoto alimkaribisha nyumbani na akala pamoja na nduguye aliebaki nyumbani (yule mkubwa) Kwa shangwe kubwa. Walakini aliebaki yule nyumbani hakumsamehe mdogowe, sawasawa na mfarisayo yule.

Kwenye mfano watatu huu tunatazamia hali ya mtu na hata ndani ya moyo wa mtu, kitu kingine tunauona ujumbe wake Kristo kwa kanisa la wakati wa mwisho.

